



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**



Simu: +255 687046147
Baruapepe: ded@kyerwadc.go.tz
Tovuti: <http://www.kyerwadc.go.tz>

S.L.P 72,
KYERWA.

13/09/2023

**TANGAZO LA UPANGISHAJI WA VYUMBA VYA BIASHARA KATIKA MJI
WA BIASHARA NKWENDA MAENEO YA STENDI MPYA YA MAGARI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa inapenda kuwakaribisha wafanya biashara wote katika Wilaya ya Kyerwa katika upangishaji wa vyumba vilivyopo maeneo ya maziwa Kata ya Nkwenda :-

Hivyo mnakaribishwa kutuma maombi ya kuomba chumba cha biashara kwenye mji huo wa Nkwenda.

SIFA ZA MWOMBAJI NI KAMA IFUATAVYO:

1. Mwombaji wa Vyumba hivyo anatakiwa kuwa mfanya biashara.
2. Mwombaji wa Vyumba hivyo anatakiwa kuwa na Leseni ya biashara iliyo hai.
3. Mwombaji anatakiwa awe na uwezo wa kukitumia chumba atakachopewa baada ya kupewa chumba hicho na asipokitumia ndani ya miezi miwili atanyang'anywa na kupewa mtu mwingine mwenye uwezo wa kukiendeleza.
4. Mwombaji atatakiwa kulipia ada ya pango isiyopungua **miezi sita** ili kuweza kupata Mkataba wa pango.
5. Mwombaji atalipia ada ya pango kiasi cha **Tshs.50,000.00** kwa mwezi, na kiwango hiki chaweza kubadilika kulingana na hali ya soko kwa wakati husika.
6. Mwombaji aambatanishe vivuli vya Leseni ya biashara, **TAX CLEARANCE** na **TIN NO.**
7. Mwombaji anatakiwa awe na kitambulisho cha uraia (**NIDA**) na kitambulisho hicho kiwe ni cha mmiliki wa kibanda cha biashara.


Mwombaji atakaye kidhi vigezo vya zabuni hiiyo ndiye atakaye itwa katika kusaini mkataba wa pande zote mbili.

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi ya Zabuni hii ni siku ya Alhamisi tarehe 28/9/2023 saa 4.00 asubuhi na Zabuni itafunguliwa muda mfupi baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi ya waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kwenye zoezi la ufunguzi wa Zabuni hizo.

Barua zote zitumwe kwa anwani ifuatayo hapa chini.

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA,
S.L.P 72,
KYERWA.**

Imetolewa


SACF. JAMES M. JOHN
MKURUGENZI MTENDAJI
HALAMSHAURI YA WILAYA
KYERWA

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KYERWA**